

## NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

4 Januari 2026

Kwa Wabahá'i wa Ulimwengu

Marafiki Wapendwa sana,

Siku tano za ushauriano wa dhati miongoni mwa Washauri wa Bara, waliokusanyika hapa katika Nchi Takatifu kwa ajili ya kongamano lao kuhusu awamu inayofuata ya Mpango wa Miaka Tisa, zimefikia tamati leo, na tunawatumia ujumbe huu mwishoni mwa mkusanyiko huu wenye baraka. Tumesikia masimulizi kutoka kwa Washauri kuhusu jitihada zenu nyingi, maendeleo yanayopatikana katika mazingira ya aina mbalimbali, na jinsi haya yalivyochangia kwenye mchakato unaoshamiri wa ujifunzaji katika kila ngazi ya jumuiya. Tumefurahishwa kwa maelezo ya jinsi ambavyo, kupitia mipangilio ya ushirikiano wa aina mbalimbali, jumuiya yenyewe inavyoibuka kama mhusika mkuu anayeonekana zaidi katika kazi ya Mpango huo. Na tumeshangazwa na yanayotokea ndani ya watu wenye kiwango cha juu kabisa cha ushiriki katika shughuli za Kibaha'i, katika maeneo ambako uhusiano wa jumuiya na jamii unazidi kuimarika na kukua kwa kasi.

Mchango mkubwa uliotolewa na Washauri wenyewe kwenye maendeleo haya, wakiongozwa kwa ustadi katika juhudi zao zote na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, ni dhahiri. Tumeguswa na umakini wa uchunguzi wao na uwazi wa tafakuri zao, vyote vikiwa vimejazwa na upendo wao ulio dhahiri kwa jumuiya wanazozihudumia. Msingi wa ushauriano wao umekuwa ni ujumbe tulioutoa kwenye kongamano lao kwenye siku yake ya ufunguzi na ambao ulitumwa mara moja kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa ili uweze kufikishwa kwenu bila kuchelewa. Ndani ya muda mfupi taarifa nyingi za uhakika zilifika kuhusu ujumbe huo ukiwa unasomwa na makundi ya marafiki wenye shauku, hata wale waliokuwa wamekusanyika kwa makusudi mengine. Tuliguswa sana na ushahidi huu ulioenea wa shauku ya kuelewa kwa haraka yale ambayo ulimwengu wa Kibaha'i umejifunza katika kipindi cha miaka minne iliyopita na kubaini nini kinapaswa kufanywa ili kuuendeleza zaidi Mpango katika miaka mitano ijayo. Hili pia litakuwa lengo la mfululizo wa mikutano ya kiasasi itakayofanyika katika miezi ijayo, ambapo bila shaka Washauri watashiriki umaizi ulioibuka kutokana na mashauriano yao ya hapa.

Kwenye Ridván, awamu ya kwanza ya Mpango wa Miaka Tisa itahitimishwa na awamu ya pili itanza. Katika kipindi hiki cha muendelezo ni muda muafaka wa kuzishirikisha roho nyingi ambazo kwa ushiriki wao Mpango ulizinduliwa miaka minne iliyopita, na ambazo idadi yao tangu hapo imeongezeka ikijumuisha marafiki wapya wasiohesabika waliovutiwa na mikutano ya ibada, shughuli za kielimu, na jitihada zingine za Kibaha'i. Tunawaalika wote kutafakari kwa pamoja, iwe katika nafasi mahsusi, kwenye mikusanyiko ya mara kwa mara ya jumuiya, au katika nyumba ya kila mmoja, juu ya yale tulijojifunza na yale tuliyoyafanikisha. Na katika kutafakari umuhimu wa shughuli hii ya kiulimwengu, tuna hakika mtaguswa pia kufikiria jinsi matendo yenu, na yale ya kaya yenu pamoja na ya jumuiya yenu, yanavyoweza kusaidia kufanikisha shabaha ya Mpango.

“Ni wajibu wa Yule wa Kweli kufunua,” Bahá’u’lláh husema, “na wajibu wa watu ni kueneza kile kilichofunuliwa.” Juhudi za dhati, za ari na anuwai zinazofanywa ili kufikisha katika kila moyo mpokevu kile ambacho Yule wa Kweli amekifunua—kutoa tumaini kwa jamii ya binadamu iliyogubikwa na taabu, kutoa njia ya kuwa mshiriki mwenye ufahamu katika kazi ya kiulimwengu ya uhuishwaji wa kiroho—ni chanzo cha kudumu cha mvuto na mshangao, cha shangwe na shukrani. Hizo ndizo hisia zinazojaza vifua vyetu wakati huu, na ambazo kwazo tutamsihi Bahá’u’lláh katika Kaburi Lake Takatifu baadaye leo awajaalie baraka kutoka neema Yake isiyo na kikomo.

*Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*